

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA ELIMU YA AWALI DARAJA LA A**

**684**

**VITENDO VYA KUJIFUNZA SANAA**

**Muda: Saa 3**

**Jumanne, 12 Mei 2015 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

### SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja mambo manne yanayoweza kumsaidia mtoto wa Elimu ya awali kupenda kuchora.
2. Katika hoja nne, oneshwa hatua za uchapaji kwa kutumia unamu wa soli ya kiatu.
3. Tofautisha maumbo ya msingi na maumbo ya upili.
4. Kwa nini vitendo vya ufinyanzi vinasisitizwa vifundishwe kwa watoto wa Elimu ya awali? Toa sababu mbili.
5. Taja vyombo au ala nne zinazoweza kupiga melodia katika muziki.
6. Elezea aina mbili za uundaji unaofaa kufundishwa kwa watoto wa Elimu ya awali.
7. Taja sifa nne za sanaa za maonesho.
8. Kwa kutoa hoja nne, ainisha umuhimu wa ufundishwaji wa ngoma kwa watoto wa Elimu ya awali.
9. Bainisha tofauti mbili kati ya soga na vichekesho.
10. Chora kielelezo cha kuimba solfa “do mi so do” na “so la ti do” katika ngazi ya kupanda na kushuka.

### SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

11. Changanua sababu tano za kufundisha mada ya uchapaji kwa watoto wa Elimu ya awali.
12. Ugizaji wa kutumia vitendo na maneno na uigizaji bubu unaathiri sana ujifunzaji wa watoto wa Elimu ya awali. Jadili.
13. Kwa kutoa hoja tano, eleza umuhimu wa kujifunza kupaka rangi kwa watoto wa Elimu ya awali.

### SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

14. Kwa mfuatano unaofaa wenye mifano madhubuti, eleza hatua tano za usimuliaji hadithi kwa watoto wa Elimu ya awali ili iwawezeshe kujifunza ipasavyo.

15. (a) Eleza mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuandaa andalio la somo.  
(b) Kwa kutoa hoja tatu, elezea umuhimu wa andalio la somo kwa mwalimu wa watoto wa Elimu ya awali.
16. Changanua maandalizi matano muhimu yanayopaswa kuchukuliwa na Mwanachuo kabla ya kwenda kwenye Mafunzo kwa Vitendo.